

TAARIFA MUHIMU KWA WATOTO WA UFALME

Dr. Godwin Gunewe

Dini na madhehebu ni matokeo ya kazi za Shetani na majeshi yake katika aidha *kuongeza kitu katika taarifa sahihi au kupunguza kitu katika taarifa sahihi au kubadilisha kabisa taarifa sahihi au kubadilisha matumizi sahihi ya taarifa sahihi husika.*

Kwa hiyo, mtu yeyote asitegemee kuwa na maisha yenye mamlaka katika dunia akiwa kwenye kikundi cha dini wala dhehebu lolote.

Ili mwanadamu awe na mamlaka katika dunia na kuwa na maisha yenye ushindi, ni lazima **kwanza abadili mtazamo wote wa nyuma yaani elimu za dini na madhehebu, aachane na mila na desturi potofu zilizo kinyume na maisha ya asili ya Ufalme na kuamini Injili ya Ufalme.** Baada ya kubadili mtazamo ni lazima mtu huyu amwamini Mfalme Yesu kwa kazi aliyoifanya ya kuurejesha Ufalme wa Mbinguni hapa duniani; na hili litamfanya mtu huyu kuzaliwa mara ya pili na Mfalme Roho Mtakatifu na kuingizwa ndani ya Ufalme.

Mtu huyu anapaswa kuendelea kujifunza habari njema ya Ufalme wa Yahweh Elohim kwa waalimu sahihi waliozamishwa na Serikali ya Mbinguni katika elimu ya Ufalme wa Mbinguni chini ya usimamizi wa Mwalimu mkuu Mfalme Roho Mtakatifu aliye ndani ya mtu husika. Mtu huyu, anapaswa kuongozwa na Mfalme Roho Mtakatifu katika kila jambo bila kuingia kwenye kikundi chochote cha dini wala dhehebu, kwa sababu kwenye vikundi vya dini na madhehebu kuna vifungo vitakavyomkosesha kutembea na maongozi ya Mfalme Roho Mtakatifu aliye ndani yake.

Mtu huyu anapaswa kuwa huru katika maisha yake ya kila siku huku akiuishi Ufalme wa Mbinguni hatua kwa hatua katika dunia. Lazima awe na mwendelezo wa

kudumu wa kujifunza kwa upana na kuziishi habari Njema ya Ufalme wa Mbinguni pamoja na miongozo, kanuni, sheria, itikadi za Ufalme wa Mbinguni hapa duniani. Mtu huyu kwa uvumilivu na ustahimilivu atakuwa anatoa matokeo hatua kwa hatua na hatimaye ataanza kuzalisha matokeo kwa ujazo na utumilifu aliokusudiwa.

Luka 8:15, *“Lakini zile mbegu kwenye udongo mzuri ni mfano wa wale **ambao hulisikia neno la Elohim na kulishika kwa moyo mnyofu na wa utii, nao kwa ustahimilivu huzaa matunda yaani huleta matokeo.**”*

Marko 4:27, *“26Pia akawaambia, “Ufalme wa Elohim unafanana na mtu apandaye mbegu shambani. 27Akiisha kuzipanda, usiku hulala na mchana huamka, nazo mbegu huota na kukua pasipo yeye kujua inavyokua. 28Udongo huifanya iote kuwa mche, halafu suke, kisha nafaka kamili kwenye suke. 29Lakini nafaka inapokuwa imekomaa, mara mkulima huingia shambani na zana za kuvunia maana mavuno yamekuwa tayari.”*

Ni nzuri kufahamu kwamba maisha ya Ufalme tunayaishi duniani kote na siyo kuungana na vikundi vya dini na madhehebu.